BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR

70 Barabara ya
Chukwani,Buyu
70490 Mjini Magharibi,
S. L. P 902 Chukwani,

Simu: +255 24 224 2000
Nukushi: +255 24 224 2000
info@zanzibarassembly.go.tz
www.zanzibarassembly.go.tz

# HOTUBA YA MAONI YA KAMATI YA USTAWI WA JAMII YA BARAZA LA WAWAKILISHI KUHUSU MSWADA WA SHERIA YA KUFUTA SHERIA YA BODI YA MIKOPO YA ELIMU YA JUU ZANZIBAR, NAM 3 YA 2011 NA KUTUNGA SHERIA YA BODI YA MIKOPO YA WANAFUNZI WA ELIMU YA JUU ZANZIBAR KWA AJILI YA KUTOA MSAADA WA KIFEDHA KWA WANAFUNZI NA MAMBO MENGINE YANAYOHUSIANA NA HAYO.

---

**Mheshimiwa Spika,**

Awali ya yote napenda nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu Mtukufu, mwingi wa rehema, aliyetujaalia uzima na afya njema na kutuwezesha kukutana leo hii ndani ya Baraza letu Tukufu kuendelea na majukumu yetu ya Kitaifa. Namuomba Mwenyezi Mungu anijaalie ufasaha katika uwasilishaji wa Hotuba hii na atupe usikivu na uelewa ili tuweze kuuchangia kwa umakini wa hali ya juu na hatimae kuupitisha mswada uliopo mbele yetu kwa maslahi ya Taifa.

**Mheshimiwa Spika,**

Kwa namna ya pekee napenda kuchukua fursa hii adhimu kukushukuru wewe binafsi kwa kuniruhusu kusimama mbele ya Baraza lako Tukufu ili niwasilishe maoni ya Kamati ya Ustawi wa Jamii ya Baraza la Wawakilishi kuhusiana na "**Mswada wa Sheria ya Kufuta Sheria ya Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu Zanzibar, Nam 3 ya 2011 na Kutunga Sheria**

**ya Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu Zanzibar kwa ajili ya Kutoa Msaada wa Kifedha Kwa wanafunzi na mambo mengine yanayohusiana na hayo”**.

**Mheshimiwa Spika,**

Kamati yangu inatoa pongeza za dhati kwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Mheshimiwa Dkt. Hussein Ali Mwinyi kwa ujasiri wake katika jukumu zima la uongozi wa Nchi hii, sambamba na jitihada anazozichukua za kuendeleza sekta ya elimu kwa lengo la kuhakikisha wanafunzi wanasoma katika mazingira yalio mazuri, hali itakayopelekea kuweza kufanya vizuri katika masomo yao.

**Mheshimiwa Spika,**

Naomba pia nichukue fursa hii kuipongeza Timu ya Wataalamu ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali kupitia Bodi ya Mkopo, kwa mashirikiano yao waliyoipatia Kamati yetu katika kipindi chote cha majadiliano ya Mswada huu, sambamba na kuwapatia mafunzo wajumbe wa Baraza ili wawe na uelewa mzuri juu ya mswaada huo.

Aidha, Napenda kuwashukuru Wanasheria wa Afisi ya Baraza la Wawakilishi pamoja na Wanasheria kutoka Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar kwa uchambuzi na ufafanuzi wa hoja mbali mbali zilizojitokeza wakati wa kuujadili mswada huu kwenye ngazi ya Kamati. Michango yao ni muhimu katika kuuboresha mswada huu kwa maslahi mapana ya nchi yetu.

**Mheshimiwa Spika,**

Fasili ndogo ya 7 ya Kanuni ya 84 ya Kanuni za Baraza la Wawakilishi, Toleo la 2020 inaipa uwezo Kamati kuwaalika Wadau mbali mbali kila

inapotokea kazi ya kujadili Miswada ya Sheria. Hivyo Kamati iliwaalika Wadau ili kutoa maoni yao juu ya Mswada uliopo mbele yetu. Kamati inathamini mchango mkubwa wa Wadau hao na inawashukuru kwa maoni na ushauri wao ulioiwezesha Kamati kutambua nafasi yao katika ukutetekelezaji wa Sheria mpya ya Bodi ya Mikopo itakayoanzishwa.

**Mheshimiwa Spika,**

Natoa pongezi za dhati kwa Wajumbe wa Kamati ya Ustawi wa Jamii kwa kazi kubwa waliyoifanya ya kuujadili na kuuchambua mswada ulioletwa mbele yao kwa upeo na ustadi wa hali ya juu. Naomba sasa niwape fursa Wajumbe wa Baraza hili kuwatambua Waheshimiwa Wajumbe wa Kamati hii mmoja baada ya mwengine kama ifuatavyo:

1. Mhe. Sabiha Filfil Thani — Mwenyekiti.
2. Mhe. Nassor Salim Ali — Makamu Mwenyekiti
3. Mhe. Bahati Khamis Kombo — Mjumbe
4. Mhe. Bihindi Hamad Khamis — Mjumbe
5. Mhe. Abdullah Hussein Kombo — Mjumbe
6. Mhe. Haji Omar Kheri — Mjumbe
7. Mhe. Salma Mussa Bilal — Mjumbe
8. Mhe. Sulubu Kidongo Amour — Mjumbe

**Mheshimiwa Spika,**

Katika uchambuzi wa Mswada huu, Kamati yangu ilifanya kazi na makatibu wetu ambao kwa kiasi kikubwa wamekuwa wakitusaidia na kuturahisishia kuuchambua ipasavyo mswada huu, naomba nao niwatambue kwa kuwataja majina yao kama ifuatavyo;

1. Ndugu Talib Enzi Talib Katibu
2. Ndugu Salha Abdulla Abdulla Katibu
3. Ndugu Bakar Makame Haji Katibu

**Mheshimiwa Spika,**

Mswada huu unalenga kuweka mazingira mazuri kwa wanafunzi wa elimu ya juu, kwa lengo la kutoa fursa za mikopo kwa wanafunzi wa Kizanzibari wenye sifa za kujiunga na masomo ya ngazi mbali mbali za elimu ya juu ndani na nje ya Nchi.

**Mheshimiwa Spika,**

Kamati yetu imefanya marekebisho kadhaa kwenye mswada huu yakiwemo marekebisho ya herufi, kuongeza aya na maneno, kufuta maneno, kuondoa makosa ya kisarufi, kuhamisha vifungu kutoka sehemu moja Kwenda sehemu nyengine, kuengeza vifungu vidogo na kuweka uwiano baina ya nakala ya mswada wa kiingereza na Kiswahili yanayoonekana kwenye waraka wa mapendekezo ya marekebisho ambao umeingizwa kwenye vishkwambi vyetu. Kimsingi, Kamati imeridhika na maudhui, dhamira na malengo ya mswada huu.

**Mheshimiwa Spika,**

Uimarishaji wa Sekta ya Elimu ni kipaumbele moja wapo cha Serikali ya Awamu ya Nane kupitia ilani ya CCM ya mwaka 2020/2025 katika ukurasa wa 231 kifungu 181 aya ya (c) ikiwa ni pamoja na kuhakikisha kuwa huduma ya upatikanaji wa Mikopo kwa vijana wetu wanaotarajia kujiunga na masomo ya elimu ya juu inatolewa katika utaratibu uliobora.

**Mheshimiwa Spika,**

Kamati imefanya marekebisho katika kifungu cha 5 katika aya ya (d) kwa kufuta maneno “**kutafuta na kusimamia**”na kuweka badala yake neno **kupokea** kwa sababu kazi ya msingi ya Bodi ni kutoa mikopo na si kutafuta ufadhili kwani hawatakua na udhibiti juu ya suala la ufadhili na udhamini wa kimasomo kwa wanafunzi.

**Mheshimiwa Spika,**

Kamati imependekeza kufanya marekekibisho katika Kifungu cha 6 kwa kuzihamisha aya ya (a), (b) na (e) kwa sababu uwezo wa Bodi wa kuamua kiwango cha kuchagua idadi ya wanafunzi, uwezo wa kuamua viwango vya mikopo na uwezo wa kuamua ada kwa huduma ni majukumu yatakayoamuliwa na Bodi ya Usimamizi. Aidha aya hizo za (a), (b) na (e) zitahamishwa kutoka kifungu cha 6 cha Mswada huu na zitahamishiwa kwenye kifungu cha 8 cha mswada huu ambapo kifungu cha 8 kinachozungumizia kazi za Bodi ya usimamizi kitakua na aya 11.

**Mheshimiwa Spika,**

Kamati imependekeza katika Kifungu cha 9 kwenye sifa za Mwenyekiti kuengeza aya mpya ya (a) itakayosomeka kama ni Mzanzibari ili kuhakikisha uzalendo juu suala la elimu unazingatiwa, sambambamba na hilo Kamati inapendekeza kuengeza vigezo vya kielemu kwani mtu atakaeteuliwa kuwa mwenyekiti wa Bodi ya usimamizi ni muhimu awe na uelewa na mambo ya kielemu au kifedha kwa sababu mambo yanahusiana na mikopo yanahitaji mtu mwenye taaluma inayolingana na mambo hayo.

**Mheshimiwa Spika,**

Kifungu cha 16 (1) (b) cha mswada huu kinalazimisha muombaji anaetaka kuomba mkopo ndani ya Bodi hii ni lazima awe amechagua

program ya mafunzo inayoendana na mpango wa vipaumbele vya Taifa. Kamati yetu inapendekeza, Pamoja na vipaumbele vya Taifa, Mnufaika asifungike kupata mkopo kwani mwanafunzi anapomaliza masomo anawajibika kurejesha mkopo huo, hivyo basi ni busara kumuachia mwanafunzi kuchagua program anayoiweza kwa sababu mwanafunzi huyo alikopeshwa na hakudhaminiwa.

**Mheshimiwa Spika,**

Kamati inapendeza kwenye suala la anaestahiki kupewa mkopo, katika kifungu cha 16 (2) Bodi ifanye tahfifu kwa wanufaika wa mkopo wa ngazi ya Stashahada na Astashahada, ukizingatia wengi wao wanatokana na familia duni. Hivyo vikiwekwa viwango sawa vya marejesho kwa wanufaika wa ngazi zote itapelekea wanufuika wa ngazi nyengine wa elimu kushindwa kuendelea na masomo ya ngazi za juu za elimu. Aidha kamati inapendekeza asilimia ya urejeshwaji kwa wanufaika wa mkopo wa ngazi Stashahada na Astashahada warejeshe angalau asilimia 10 ya mkopo ili waweze kuendelea na masomo ya ngazi za juu ya kielimu, na kiwango hicho cha asilimia kianishwe kwenye sheria na sio kwenye Kanuni kama inavyosomeka sasa.

**Mheshimiwa Spika,**

Kamati inapendekeza katika kifungu 23 cha Mswada huu kuengezwa kifungu kidogo cha (2) kipya kitachozungumzia urejeshwaji wa mikopo bila riba, kitakachosomeka kama ifuatavyo:

**"Bila ya kujali masharti ya sheria nyengine yoyote, mkopo utakaotolewa chini ya sheria hii, marejesho yake hayatakuwa na riba".**

Sababu ya mabadiliko ya kifungu hicho ni kuwapunguzia mzigo wanufaika wa mkopo wakati wanapofanya marejesho.

**Mheshimiwa Spika,**

Kamati inapendekeza kufanya marekibisho katika Kifungu cha 33 katika kifungu kidogo cha 2 kama ifuatavyo:

**"Kwa kuzingatia masharti ya Sheria ya Usimamizi wa Fedha za Umma, Nam 12 ya 2016 Bodi inaweza wakati wowote kuandaa bajeti ya ziada kwa mwaka wa fedha unaoendelea na kuiwasilisha kwa Bodi ya Usimamizi kwa kupata ridhaa na kuiwasilisha kwa Waziri".**

Sababu ya kufanya marekebisho hayo ni kuipa uwezo Bodi ya usimamizi katika kusimamia utekelezaji wa kazi za Bodi ikiwemo pia kusimamia Bajeti za ziada.

**Mheshimiwa Spika,**

Kamati inaiomba wizara ya Fedha na Mipango kuwaingizia fedha Bodi ya Mikopo kwa wakati ili kuepusha malalamiko ya kucheleweshewa kupata huduma kwenye vyuo wanavyosoma wanafunzi ili lile lengo lilokusudiwa la kuboresha huduma liweze kufikiwa.

**Mheshimiwa Spika,**

Kufuatia kilio cha wanafunzi kulipia mkataba kila mwaka mpya wa masomo, wengi wao hushindwa kulipia gharama hizo kwa sababu hali zao ni duni. Hivyo, Kamati inashauri Bodi watengeneze mfumo wa kujaza mkataba kwa njia ya kielektroniki katika kupokea fedha za kujikimu ili kuepuka ucheleweshaji wa kupata fedha hizo na ujazaji wa mkataba huo ufanyike mara moja tu anaposajili mkopo kwa mara ya mwanzo na si vyenginevyo.

**Mheshimiwa Spika,**

Napenda nimalizie kwa kuishauri Wizara kwa vile kumekuwa na vifungu

kadhaa vinavyohitaji uwepo wa Kanuni, Kamati inashauri kuharakisha utungwaji wa Kanuni hizo mapema ili kanuni hizo ziweze kwenda sambamba na marekebisho ya Sheria mpya itakayoanzishwa na kuviwezesha vifungu vya Sheria hiyo kuweza kutekelezeka kwa ufanisi.

**Mheshimiwa Spika,**

Kamati imetowa mapendekezo mbali mbali kwa ajili ya kuuboresha mswada huu ili uweze kutoa huduma zilizo bora ambazo zitakwenda kumnufaisha mwanafunzi aliyepata fursa ya kujiunga na chuo.

Pia marekebisho mengine yaliyopendekezwa na Kamati ya Ustawi wa Jamii yameainishwa kwenye waraka wa marekebisho ambao tayari umeingizwa kwenye mfumo wa Baraza mtandao.

**Mheshimiwa Spika,**

Kwa kumalizia, natoa shukurani za dhati kwa Wajumbe wote wa Baraza lako Tukufu kwa utulivu na usikivu wao wakati wote wa uwasilishaji wa taarifa hii, naomba tuuchangie, tuujadili, tutowe mapendekezo na hatimae tuupitishe mswada huu.

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Kamati yangu, naomba kuwasilisha.

Ahsante,

……………………………
Mhe. Sabiha Filfil Thani,
Mwenyekiti,
Kamati ya Ustawi wa Jamii,
Baraza la Wawakilishi,
**Zanzibar.**